FUNZO LA 22

1.  Je, Mungu alijua kuhusu uovu wa watu wa Sodoma na Gomora?
-Ndiyo.

2.  Je, watu wakimsahau Mungu, Mungu atawasahau?
-La.

3.  Je, watu wakimsahau Mungu, Mungu atasahau dhambi zao?
-La.

4.  Je, kwa nini ni lazima Mungu aadhibu kila dhambi?
-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.
-Kwa sababu Mungu aliwaumba watu wakamilifu.
-Kwa sababu kila dhambi inapinga Mungu.

5.  Je, ni kwa nini Mungu hakuwaadhibu papo hapo watu wa Sodoma na Gomora kwa dhambi zao?
-Kwa sababu Mungu alitaka watubu dhambi zao.
-Kwa sababu Mungu alitaka kuwaokoa.

6.  Je, ni kwa nini Mungu hawaadhibu watu papo hapo kwa dhambi zao?
-Kwa sababu Mungu anataka watubu dhambi zao.
-Kwa sababu Mungu anataka kuwaokoa.

7.  Je, Mungu huwatisha watu tu, ila hawaadhibu kwa dhambi zao?
-La.



-Mungu ataadhibu kila dhambi.

8.  Je, unapofika wakati wa Mungu kuwaadhibu wenye dhambi, kuna yeyote anayeweza kumzuia Mungu?
-La.

9.  Kama vile dhambi ilivyomvuta Lutu Sodoma, je, dhambi huwafanyia nini watu wote?
-Dhambi huwavuta watu karibu na uovu wake.

10.  Je, tunalingana aje na watu wa Sodoma na Gomora?
-Tumenena uongo mwingi, mwingi sana.
-Tumewashuhudia wengine uongo.
-Tumewalaani majirani wetu.
-Tumeiba vitu vya watu wengine.
-Tumelala na wake wa waume wengine.
-Tumewaua wenzetu.

11.  Je, kwa nini Mungu alimwokoa Lutu?
-Kwa sababu Lutu alijua kuwa alimtendea Mungu dhambi.
-Kwa sababu Lutu alijua kuwa dhambi yake ilileta kifo cha milele.
-Kwa sababu Lutu alijua kuwa ni Mungu pekee angeweza kumwokoa.
-Kwa sababu Lutu aliamini kuwa Mungu angemtuma Mwokozi amwokoe.

12.  Je, ni kwa nini Mungu alimgeuza mke wa Lutu akawa nguzo ya chumvi?
-Kwa sababu mke wa Lutu hakumtii Mungu, aliangalia nyuma.

13. Je, kwa nini mke wa Lutu aliangalia nyuma?
-Kwa sababu alipenda dhambi yake.
-Kwa sababu hakutaka kuwacha dhambi yake.

-Mungu aliahidi kuwapa Ibrahamu na Sara mwana.

-Ibrahamu alikuwa miaka 100 na Sara miaka 90, ilhali hawakuwa na watoto.

-Je, Mungu alisahau ahadi yake ya kumpa mwana?
-La.

-Mungu awezi sahau ahadi zake.
-Mungu hutimiza ahadi zake.

-Je, Mungu alibadilisha mawazo yake ya kumpa Ibrahamu mwana?
-La.

-Mungu hawezi badilisha mawazo yake.
-Mungu hufanya kile ameahidi kufanya.

-Abrahamu alikuwa miaka 100 na Sara miaka 90 na walikuwa tasa.

-Je, ilikuwa ni vigumu kwa Mungu kuwapa Ibrahamu na Sara mwana?
-La.

-Hakuna kilicho kigumu kwa Mungu.



-Mungu anaweza kufanya chochote.

-Kama vile Mungu alivyoahidi, aliwapa Ibrahamu na Sara mwana.

Tusome Mwanzo 21:1-3

1-Bwana akamjia Sara kama alivyonena, na Bwana akamfanyia kama alivyosema.
2-Sara akapata mimba akamzalia Ibrahimu mwana wa kiume katika uzee wake, kwa muhula alioambiwa na Mungu.
3-Ibrahimu akamwita jina lake Isaka, yule mwana aliyezaliwa, ambaye Sara alimzalia.

-Je, iliwezekanaje kwa Ibrahamu aliyekuwa miaka 100 na Sara miaka 90 na tasa kuzaa mwana?

-Kwa sababu ni Mungu anayepeana uhai.
-Kwa sababu Mungu anaweza fanya chochote.

-Je, aliitwaje mwana ambaye Mungu aliwapa Ibrahamu na Sara?
-Isaka.

-Baada ya miaka mingi, Isaka alikuwa na akawa kijana mwenye nguvu.
-Ibrahamu na Sara walimpenda Isaka sana.

-Je, Ibrahamu alijua kuwa Mungu alipanga kumleta Mwokozi kupitia kizazi cha Isaka?

-Ndiyo.

-Abrahamu alikumbuka ahadi ya Mungu ya kumleta Mwokozi kupitia kizazi cha Isaka.

-Siku moja, Mungu alinena na Ibrahamu kumhusu Isaka.

Tusome Mwanzo 22:1-2

1-Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa.

2-Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia.

-Je, kwa nini Mungu alimwamuru Ibrahamu amtoe sadaka Isaka?
-Mungu alitaka kumjaribu Ibrahamu.

-Je, kwa nini Mungu alitaka kumjaribu Ibrahamu?
-Mungu alitaka kuona kama Ibrahamu alimpenda Mungu zaidi ya Isaka.

-Je, kwa nini Mungu alimwamuru Ibrahamu amtoe Isaka kama sadaka?

-Kwa sababu Mungu alimpa Ibrahamu uhai.
-Kwa sababu Mungu alimpa Isaka uhai.



-Kwa sababu Mungu ni Bwana wa watu wote.

-Je, jirani yako humwambia mke wako anachofaa kufanya?
-La.
-Kwa nini?
-Kwa sababu jirani yako sio bwana wa mke wako.

-Je, jirani yako huamua jinsi utakavyopanda shamba lako?
-La.
-Kwa nini?
-Kwa sababu jirani yako sio bwana wa shamba lako.

-Je, Bwana wa Ibrahamu ni nani?
-Mungu.

-Je, bwana wa watu wote ni nani?
-Mungu.

-Kwa sababu Mungu ni Bwana wa watu wote, Mungu anaweza kuwaamuru watu wote kufanya chochote anachotaka.

-Mungu alipomwamuru Ibraham kumtoa Isaka sadaka, Ibrahamu alifanya nini?

Tusome Mwanzo 22:3

3-Ibrahimu akaondoka alfajiri, akatandika punda wake, akachukua vijana wawili pamoja naye, na Isaka mwanawe, akachanja kuni kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka, akaenda mpaka mahali alipoambiwa na Mungu.

-Ibrahamu alikata kuni za sadaka, akamchukuwa Isaka na wajakazi wake wawili kuelekea mahali ambapo Mungu angemwonyesha.

-Ibrahamu angemtoaje Isaka sadaka?

-Je, iwapo Ibrahamu angemtoa Isaka sadaka, Mungu angetimiza vipi ahadi zake?

-Je, iwapo Ibrahamu angemtoa Isaka sadaka, Mungu angewezaje kumpa Ibrahamu uzao mwingi?

-Je, iwapo Ibrahamu angemtoa Isaka, Mungu angewazaje kumtuma mwokozi kupitia uzao wa Ibrahamu?

-Mungu alimuahidi Ibrahamu kuwa Isaka atakuwa baba wa uzao mwingi na kuwa Mwokozi atakuwa mzao wake.

-Je, Mungu alibadilisha mawazo yake?
-La.
-Je, Mungu aliamua kuvunja ahadi zake?
-La.
-Je, Ibrahamu aliwaza kuwa Mungu alibadili mawazo yake?
-La.

-Ibrahamu alimwamini Mungu na ahadi zake.
-Ibrahamu aliamini kuwa Mungu angetimiza ahadi zake.

-Ibrahamu aliamini kuwa Mungu angetimiza ahadi yake ya kumpa uzao mwingi.



-Ibrahamu aliamini kuwa Mungu angetimiza ahadi yake ya kumtuma mwokozi.

-Ibrahamu aliamini Mungu angefanya nini kama angemtoa Isaka kafara?

-Ibrahamu aliamini kuwa kama angemtoa Isaka kafara, Mungu angemfufua Isaka kutoka kwa wafu.

-Kuamini kwa Ibrahamu kulikuwa tofauti na kule kwa Adamu na Hawa.

-Katika Bustani ya Edeni, Mungu aliwaambia Adamu na Hawa kuwa wangekufa kama wangekula kutoka kwa Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya.

-Adamu na Hawa hawakumwamini Mungu.
-Lakini Ibrahamu alimwamini Mungu.

-Kwa sababu Ibrahamu alimwamini Mungu, alimchukuwa Isaka pamoja na wajakazi wake wawili na kuelekea pahali ambapo Mungu angemwonyesha.

Tusome Mwanzo 22:4-6a

4-Siku ya tatu Ibrahimu akainua macho yake, akapaona mahali pakali mbali.
5-Ibrahimu akawaambia vijana wake, Kaeni ninyi hapa pamoja na punda, na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kuwarudia tena.

6-Basi Ibrahimu akazitwaa kuni za hiyo sadaka, akamtwika Isaka mwanawe;

-Ibrahamu na Isaka walipokuwa wakitembea pamoja, Isaka alimuuliza babake swali.

Tusome Mwanzo 22:6b-7

6-Akatwaa moto na kisu mkononi mwake, wakaenda wote wawili pamoja.
7-Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babangu! Naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?

-Je, swali la Isaka lilikuwa lipi?
-"Yuko wapi mwana kondoo wa kutolewa sadaka?"

-Isaka alijua kuwa babake alikuwa anaenda kutoa sadaka.
-Isaka alijua kuwa walikuwa wamebeba moto na kuni.

-Ila Isaka hakuelewa sababu ya wao kutokumchukuwa mwana kondoo.

-Je, Ibrahamu alimjibu vipi Isaka?

Tusome Mwanzo 22:8

8-Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote wawili



pamoja.

-Je, Ibrahamu alimjibu vipi?
-Abrahamu alijibu kuwa Mungu mwenyewe angejitwalia mwana kondoo.

-Ibrahamu aliamini kuwa Mungu angetwaa kafara.

-Kumwamini Mungu ndiyo kazi muhimu zaidi ambayo tunaeza fanya.

-Kusikiliza tu ujumbe wa Mungu huwezi kutuokoa.
-Lazima tuamini ujumbe wa Mungu ili tuokoke.

-Ufuatao ni mfano:

-Mtu mmoja alikuwa mgonjwa sana na akaenda kumuona daktari.

-Daktari alimwangalia yule mtu, na akamwambia ugonjwa aliokuwa nao.

-Kisha, daktari alimpa yule mgonjwa dawa ambazo aliitaji ili awe na afya tena.

-Yule mtu alizichukuwa zile dawa, akaziweka mfukoni na akarejea nyumbani.

-Ila, huyo mgonjwa hakuzimeza zile dawa.

-Yule mgonjwa alimsikiliza tu dakatari.
-Hakuzimeza zile dawa.

-Je, huyo mgonjwa angepona?
-La.

-Kusikiliza tu neno la Mungu hakuwezi kukuokoa.
-Lazima uamini neno la Mungu kama Ibrahamu.

-Kama utasikiliza tu ujumbe wa Mungu, ila usiamini, utakuwa kama Shetani.

-Kama utasikiliza tu ujumbe wa Mungu, ila usiamini, utakuwa unamuita Mungu muongo.

-Mungu huwaokoa wale tu wanaomwamini.
-Mungu huwaokoa tu wanaoamini Neno lake.

-Neno la Mungu liko wapi?
-Katika Kitabu cha Mungu, Biblia.

-Ibrahamu na Isaka wakafika mahali ambapo Mungu aliwaonyesha, nini kikafanyika?

Tusome Mwanzo 22:9-10

9-Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni.



10-Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe.

-Je, Ibrahamu alifanya nini?
-Alimfunga Isaka na kumuweka juu ya madhabahu.

-Je, Ibrahamu aliweza kumuokoa Isaka?
-La.
-Kwa nini Ibrahamu hangeweza kumuokoa Isaka?

-Kwa sababu Ibrahamu alikuwa tayari amekiinua kisu ili amtoe Isaka kafara.

-Je, Isaka angeweza kujiokoa?
-La.
-Kwa nini Isaka hangeweza kujiokoa?

-Kwa sababu Ibrahamu alikuwa ameifunga miguu na mikono ya Isaka.

-Isaka hangeweza kutoroka.

-Mungu alipotuma mafuriko, watu walifungiwa nje ya mashua hawakuweza kutoroka.

-Mungu alipotuma moto kutoka mbinguni, watu wa Sodoma na Gomora hawakuweza kutoroka.

-Mke wa Lutu alipotazama nyuma kuelekea mji wa Sodoma, hakuweza kutoroka.

-Hakuna anayeweza kutoroka.

-Je, ni nani pekee aliyeweza kumuokoa Isaka?
-Mungu.

-Je, watu wengine wanaweza kutuokoa?
-La.
-Je, tunaweza kujiokoa?
-La.

-Je, ni nani pekee anayeweza kutuokoa?
-Mungu.

-Mungu pekee ndiye aliyemuokoa Nuhu na jamii yake.
-Mungu pekee ndiye aliyemuoka Lutu na binti zake wawili.

-Mungu pekee ndiye anayeweza kuokoa watu wote.
-Mungu pekee ndiye aliyeweza kumuokoa Isaka.

-Je, Mungu alimuokoa Isaka?

Tusome Mwanzo 22:11-12

11-Ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa.

12-Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee.



-Je, ni nani aliyemuongelesha Ibrahamu na kumuokoa Isaka?
-Mungu.

-Mungu pekee ndiye aliyemzuia Ibrahamu asimuue Isaka.
-Mungu pekee ndiye aliyemuokoa Isaka.

-Lakini Isaka hangeokolewa kama hakungekuwa na kafara nyingine.

-Je, Ibrahamu alikuwa na sadaka nyingine?
-La.

-Je, Isaka alikuwa na sadaka nyingine?
-La.

-Je, Mungu alifanya nini?

Tusome Mwanzo 22:13

13-Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe.

-Ibrahamu hakuwa na sadaka nyingine.
-Isaka hakuwa na sadaka nyingine.

-Je, ni nani aliyetwaa sadaka ambayo ilichukuwa sehemu ya Isaka?
-Mungu.

-Mungu pekee ndiye aliyetwaa sadaka.

-Je, ni sadaka gani ambayo Mungu alitwaa?
-Kondoo wa kiume.

-Alikuwa wapi huyo kondoo?
-Alikuwa amenaswa katika kichaka kwa pembe zake.

-Je, kwa nini kondoo alinaswa kwa pembe zake kichakani?
-Kwa sababu Mungu alimfunga huyo kondoo.

-Je, kwa nini Mungu alimfunga huyo kondoo kwa pembe zake?

-Kwa sababu Mungu angekubali sadaka kamilifu pekee kuchukuwa sehemu ya Isaka.

-Kama yule kondoo angefungwa kwa kichwa au miguu, angejiumiza kwa kujaribu kutoroka.

-Mungu ni mkamilifu.
-Mungu atakubali sadaka kamilifu pekee.

-Ibrahamu akamfungua Isaka na kumfunga kondoo aliyetwaliwa na Mungu katika madhabahu.

-Ibrahamu akamtoa yule kondoo sadaka badala ya Isaka.

-Yule kondoo akafa badala ya Isaka.
-Yule kondoo alichukuwa sehemu ya Isaka.



-Je, Ibrahamu alipaitaje pahali ambapo Mungu alijitwalia kondoo?

Tusome Mwanzo 22:14-19

14-Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire,kama watu wasemavyo hata leo,Katika mlima wa BWANA itapatikana.
15-Malaika wa Bwana akamwita Ibrahimu mara ya pili kutoka mbinguni
16-akasema, Nimeapa kwa nafsi yangu asema Bwana, kwa sababu umetenda neno hili, wala hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee,
17-katika kubariki nitakubariki, na katika kuzidisha nitauzidisha uzao wako kama nyota za mbinguni, na kama mchanga ulioko pwani; na uzao wako utamiliki mlango wa adui zao;
18-na katika uzao wako mataifa yote ya dunia watajibarikia; kwa sababu umetii sauti yangu.
19-Basi Ibrahimu akawarudia vijana wake, wakaondoka, wakaenda zao pamoja mpaka Beer-sheba; Ibrahimu akakaa huko Beer-sheba.

-Ibrahamu alipaita pahali ambapo Mungu alijitwalia kondoo, “Mungu atatwaa.”

-Je, kwa nini Ibrahamu alipaita hapo pahali, “Mungu atatwaa”?

-Ibrahamu aliamini kuwa, kama vile Mungu alivyojitwalia kondoo, hivyo ndivyo atatwaa Mwokozi awaokoe watu.